

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

Simu Na. (025) 2520121  
2520109, 2520035  
Fax Na. (025) 2520117  
Barua pepe:  
ded.chunya@mbeya.go.tz  
Unapojuibu tafadhalii taja:  
Kumb. Na. CDC/  
S.10/39/VOL.III/42



S.L.P. 73,  
CHUNYA

Tarehe: 21/03/2018

**YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa watanzania wenyewe sifa na uwezo wa kujaza nafasi za kazi kama ifuatavyo Afisa Mtendaji wa Kijiji daraja la III.

**MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III (Nafasi 19)**

**(a) Sifa za Muombaji**

Kuajiriwa mwenye Elimu ya kidato cha nne au sita na aliyehitimu Mafunzo ya Astashahada/cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa, kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**(b) Mshahara**

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali ngazi ya Mshahara TGS B.

**(c) Majukumu ya Kazi**

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji;
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji;
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji;
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, sharia na Taratibu;
- vi. Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lako na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza usalishaji mali;
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalamu katika Kijiji;

- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji;
- ix. Mwenyekiti wa kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji;
- x. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi;
- xi. Kusimamia utungaji wa sharia ndogo za Kijiji na
- xii. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

#### **4 MASHARTI YA JUMLA**


- Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wenyе umri kuanzia miaka 20 hadi 45.
- Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingia katika kada tofauti walizonazo, wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa waajiri wao.
- Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (**Detailed CV**) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (3) wa kuaminika.
- Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma na vyeti vya kidato cha nne au sita kwa wale waliofika kiwango hicho na wenyе vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia kazi husika. Pia iambatanishwe picha ndogo (**passport size**) ya hivi karibuni na iandikwe majina matatu nyuma yake.
- Testimonials, provision results, statement of results na hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (form four & form six) **HAVITAKUBALIWA**.
- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na Mamlaka husika (**NECTA, NACTE na TCU**).
- Waombaji waliostaafishwa katika utumishi wa Umma hawataruhusiwa kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- Uwasilishaji wa sifa za **kughushi** wahusika watachukuliwa hatua stahiki za kisheria.
- Maombi yaandikwe kwa mkono na muombaji kwa lugha ya Kiswahili au kiingereza.
- Waombaji wote kwenye barua zao za maombi waandike namba za simu za uhakika kwa ajili ya mawasiliano.

Maombi yote yatumwe kwa anuani ya posta kama ifuatavyo:-

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA,  
S.L.P. 73,  
CHUNYA.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 04/04/2018 saa 9.30 Alasili.

Imetolewa na

  
**Sophia J. Kumbuli**  
**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA**  
**CHUNYA**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
CHUNYA**